BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Tatu – Tarehe 17 Februari, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

128. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Licha ya kuundwa kwa Kamati iliyojumuisha wataalamu kutoka Wizara mbali mbali za Serikali, kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa kitaalamu kuhusiana na tatizo la kujaa kwa maji kwenye eneo la Meli Nne 'High Perfomance' na mzunguko wake *zone "f"*, tatizo hilo bado halijatatuka na wala ripoti ya Kamati hiyo haijawekwa hadharani.

(a) Je, ni lini Serikali italishughulikia eneo hili, ili kuwaondoshea wananchi usumbufu wa kuingiliwa na maji majumbani mwao.

(b) Je, ni sababu zipi zilizopelekea Kamati iliyoundwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kushindwa kutupatia ripoti ya kitaalam ya uchunguzi wa eneo hilo kwa muda mrefu sasa.

(c) Nini kauli ya Serikali kwa hatua za dharura na za muda ujao wa kuondokana na kadhia hii ya muda mrefu sasa.

<u>Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:</u>

53. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Pamoja na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya ya Zanzibar, bado utumiaji wa dawa za kulevya umekuwa kero kubwa nchini. Ongezeko lake huathiri ukuwaji wa maendeleo nchini. Hata hivyo, baadhi ya wananchi hulalamika kuwa, Serikali yetu bado haijaipa Mamlaka hiyo kipaumbele kinachostahiki:

(a) Je, Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya ina mahitaji gani ya wataalamu na nyenzo ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(b) Je, ni lini Serikali itaikamilishia Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya mahitaji yake ya lazima ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>

66. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Naipongeza Serikali kwa kuwajali na kuendelea kuwajengea mazingira mazuri wajasiriamali wetu.

Je, nini kifanyike ili kuwafanya wananchi kuzithamini bidhaa zinazozalishwa na wajarisiamali wetu na kuzinunua ili kuikuza sekta hii ya ujasiriamali.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

165. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na juhudi kubwa za kukusanya mapato, kitendo cha Manispaa, Mabaraza ya Miji au Halmashauri kukusanya mapato yatokanayo na maegesho ya magari na vyombo mbali mbali vya moto katika maeneo mbali mbali nchini, bila ya kuyaboresha maeneo hayo, hakileti taswira nzuri na kuthibitisha kuwa Serikali inakusudia kutoa huduma bora kwa wenye magari na vyombo hivyo.

(a) Je, kwa nini Serikali inakusanya mapato ya maegesho ya magari na vyombo mbali mbali vya moto bila ya kuyaboresha maeneo ya maegesho hayo.

(b) Je, Serikali inayatumia kwa shughuli gani mapato yanayopatikana kutokana na maegesho hayo.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

23. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa maendeleo yote duniani yanategemea sana namna ya nchi hiyo inavyoenzi utamaduni wake. Na kwa kuwa, elimu inayofunzwa katika nchi husika kupitia mitaala yao, ndio inayopelekea sana kufahamika na kuenzika kwa utamaduni wa nchi hiyo.

(a) Je, kwa kiwango gani Wizara yako inashirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuulinda na kuuhifadhi utamaduni wetu kupitia mitaala inayosomeshwa na Wizara hiyo.

(b) Je, Wizara yako imejiridhishaje kama mitaala inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina ufanisi katika kuulinda, kuuhifadhi na kuurithisha utamaduni wetu kwa vizazi vijavyo.

(c) Je, Wizara yako imewahi kutoa michango gani katika kuandaliwa kwa mitaala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inayohusiana na utamaduni wetu na kwa uthibitisho gani kuwa michango yako hiyo imekubaliwa na Wizara hiyo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

13. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Pamoja na juhudi kubwa za Serikali za kuongeza ajira kwa wananchi mbali mbali Unguja na Pemba, wananchi wengi wanafurahia kupata ajira za kudumu kuliko ajira za muda ama za mkataba, kutokana na usalama wa ajira za kudumu.

(a) Kwa nini wafanyakazi wengi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wanafanya kazi zao kwa mkataba.

(b) Kwa nini wafanyakazi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wanakuwa na mikataba ya muda mrefu bila ya kuajiriwa kwa ajira za kudumu.

97. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi kubwa za kujenga miundombinu mbali mbali nchini, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara. Hata hivyo, barabara inayokwenda JKU Chambani haiko katika hali nzuri kwa muda mrefu sasa, bila ya kufanyiwa matengenezo.

Je, Wizara kupitia Baraza la Mji ina mpango gani wa kuitengeneza angalau kwa kifusi barabara hiyo, kutoka Chakalakati hadi ilipo kambi ya JKU Chambani.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

151. MHESHIMIWA AZA JANUARI JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga skuli nyingi bora na za kisasa. Hata hivyo, bado kuna changamoto mbali mbali zinazoikabili sekta ya elimu kupitia skuli hizo.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba skuli hizo zinaongeza ufaulu kwa wanafunzi wake.

(b) Katika skuli binafsi zinaonekana kuchukua juhudi za makusudi za usomeshaji ili kuhakikisha wanaongeza ufaulu kwa wanafunzi wao na pindipo mwalimu atajulikana kuwa hana juhudi huadhibiwa na wakati mwengine hata kufukuzwa kazi. Je, suala hili likoje kwa upande wa Wizara yako.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

18. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa suala la kilimo cha biashara ni moja kati ya vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuanguka kwa kilimo cha mpira hapa Zanzibar.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kukianzisha na kukiendeleza kilimo cha mpira katika maeneo mbali mbali nchini.

(c) Kwa kuwa mpira ni miongoni mwa bidhaa zenye soko kubwa. Je, Wizara ina mikakati gani ya kusimamia uzalishaji wa bidhaa ya mpira.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

71. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Mashamba ya Wakfu yamekuwa yakifuata utaratibu uliopangwa kwa mujibu wa Kanuni za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar. Aidha, utaratibu wa mashamba yanayowekwa wakfu na wananchi wakati wa uhai wao ni kuendelezwa kwa wakfu huo mara tu baada ya kufariki dunia, ili kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza katika familia zinazowekewa wakfu huo.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea mashamba hayo ya wakfu kuchelewa kuwanufaisha walengwa baada ya mrithiwa kufariki dunia.

(b) Je, ni sababu zipi zimepelekea kwa baadhi ya kesi za mirathi hasa mashamba yanayowekwa wakfu kushindwa kumalizika kwa muda mfupi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Kadhi.

(c) Je, ni mashamba mangapi hadi sasa yameshakabidhiwa kwa walengwa kwa kuzingatia usia wa marehemu wa kuwekwa shamba lake wakfu.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

110. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Tunakotoka kulikuwa na utaratibu wa watalii wetu wanaoingia nchini pamoja na wageni wengine kuwa na miongozo maalum juu ya mavazi yanayoendana na silka halisi za Mzanzibari kwa lengo la kuilinda jamii husika.

(a) Je, miongozo hiyo ya awali imeondolewa.

(b) Kama haijaondolewa, kwa nini watalii walio wengi wanapoingia nchini hawaifuati miongozo hiyo na kupelekea baadhi yao kutembea isivyo rasmi.

(c) Je, Wizara yako imeandaa muongozo wowote wa mavazi kwa watalii wanaoingia nchini, tokea kuanza kwa Awamu hii ya Nane.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**17 Februari, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**